

TAARIFA YA KANISA ANGLIKANA TANZANIA KWA UMMA JUU YA KIFO CHA MWINJILISTI BILL GRAHAM (1918-2018)

Kanisa Anglikana limepokea taarifa za kifo cha Mwinjilisti mashuhuri duniani wa karne ya 20 Mwinjilisti Bill Graham kwa masikitiko na kwa kutiwa moyo kwa huduma yake. Akitoa taarifa juu ya kifo chake, mtoto wa marehemu amesema "Baba yangu aliwahi kuulizwa kuwa mbinguni ni wapi, alijibu kuwa mbinguni ni mahali alipo Yesu na siku nikifa nitakwenda kuishi naye." Mwinjilisti Graham amepumzika maisha ya hapa dunuani lakini anaishi katika tumaini la ufufuo wa wafu. Anaishi na Kristo katika tumaini la wokovu wetu.

Wahudumu wengi wa Kanisa Anglikana wameelezea jinsi Bill Graham alivyochangia katika wokovuna imani yao. Anakumbukwa sana alipofanya safari yake mjini Moshi Tanzania na hotuba zake kukarimaniwa na Askofu Festo Kivengere kwenye miaka ya 1960. Askofu Festo Kivengere alifanyakazi katika shule ya Alliance Secondary (baadae ilikuja kujulikana kama Shule ya Sekondari ya Mazengo), ambacho sasa ni Chuo Kikuu cha Kanisa Anglikana Tanzania cha Mtakatifu Yohana (St John's University) cha mjini Dodoma.

Kanisa Anglikana Tanzania linathibitisha kwamba maisha na huduma ya Bill Graham ni ushahidi wenye utukufu kwa kanisa. Tunaungana na waumini wote duniani wanao adhimisha kifo cha Bill Graham kwa kutoa salamu za upendo kwa familia na taasisi zinazoendele za urithi wa huduma yake.

Askofu Francis Ntiruka (Askofu mstaafu wa Kanisa Anglikana Dayosisi ya Tabora), akielezea kupokea taarifa za Bill Graham amesema "kifo chake kimetushtusha lakini tunamshukuru Mungu kwa kazi nzuri aliyofanya bila ubaguzi. Alikuwa mtu wa watu wengi wadogo kwa wakubwa na alihubiri injili kwa uaminifu na urahisi. Na taasisi yake haikuwa na kashfa za fedha wala maadili mabaya ya ndoa." Bill Graham alikuwa mhubiri wa kweli na Kanisa Anglikana Tanzania linaungana na waumini wote walioguswa na maisha ya miaka 99 ya Bill Graham, kumpa Mungu shukrani kwa uaminifu wake. Bill Graham ni zawadi yetu.

Imesainiwa na

Rev.Can. Dr Mecka Ogunde
KATIBU MKUU – KANISA ANGLIKANA TANZANIA.

ANGLICAN CHURCH OF TANZANIA

PRESS RELEASE ON THE DEATH OF EVANGELIST BILL GRAHAM (1918 – 2018)

The Anglican Church of Tanzania has received the news of death of the 20th century world famous evangelist Bill Graham with great sorrow but also with inspiration for his ministry. Announcing his death, son of the deceased said, "My father was once asked where heaven is, he answered that heaven is where Jesus Christ is and when I die I will go and live with him". Evangelist Graham rested in peace from physical life but he still lives in hope of resurrection.

Number of ministers in the Anglican church of Tanzania expressed how Bill Graham contributed in their spiritual rebirth and faith. He will be remembered during his trip to Moshi town in Tanzania in 1960's, when Bishop Festo Kivengere translated his speeches. Bishop Festo Kivengere worked with Alliance Secondary (later became known as Mazengo Secondary School), which is now St. John's University in Dodoma, a University of the Anglican Church of Tanzania

The Anglican Church of Tanzania endorses the life and ministry of Bill Graham as glorified truth to the church. The church joins believers worldwide in remembering the death of Bill Graham by delivering kindness greetings to the family and institutions that inherited his ministry.

When receiving the news about his death, Bishop Francis Ntiruka (retired Bishop of the Anglican church of Tanzania, Diocese of Tabora) said "his death come as a shock to many of us but we thank God for his ministry. He stands for everyone, young and elders and he preached the gospel in simple ways. His organization never had neither money scandals nor bad marriage manners". Bill Graham was a true minister and that the Anglican Church of Tanzania joins all believers that have been touched by the life of Bill Graham throughout his 99 yrs. to thank God for his trust. Bill Graham is our gift.

Signed by

Rev. Can. Dr. Mecka Ogunde

General Secretary – Anglican Church of Tanzania.